# Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Morogoro




# Mdahalo wa Kitaifa wa Kumbukizi ya Miaka 40 ya Edward Moringe Sokoine

08 Aprili 2024
Kampasi ya Edward Moringe
Morogoro

# Mdahalo wa Kitaifa wa Kumbukizi ya Miaka 40 ya Edward Moringe Sokoine

**Kauli mbiu:** *"Kumbukizi ya Miaka 40 ya Edward Moringe Sokoine: Urithi wa Taifa katika Uongozi wake, Bidii, Uadilifu na Uaminifu"*

## 1.0 Utangulizi

### 1.1 Muktadha wa Kumbukizi na Umuhimu wake

Kongamano la kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine lilifanyika ili kuenzi mchango mkubwa wa Hayati Edward Moringe Sokoine kwa Taifa la Tanzania. Kumbukizi hii ni muhimu kwa sababu inatukumbusha uzalendo, uadilifu, na uaminifu aliouonesha wakati wa uongozi wake. Pia, inatoa fursa kwa kizazi kipya kuelewa na kuthamini mchango wa Hayati Sokoine katika maendeleo ya nchi, hususan katika sekta ya kilimo.

### 1.2. Muhtasari Kuhusu Hayati Edward Moringe Sokoine


***Hayati Edward Moringe Sokoine***

Hayati Edward Moringe Sokoine alikuwa Waziri Mkuu wa Tanzania chini ya serikali ya awamu ya kwanza iliyoongozwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Alishika nyazifa mbalimbali serikalini na alihudumu kama Waziri Mkuu kwa vipindi viwili, kwanza toka mwaka 1977 hadi 1980, na pili toka mwaka 1983 hadi 1984. Katika kipindi chake cha uongozi, Sokoine alisimamia na kupigania maendeleo ya sekta mbalimbali nchini, hususan sekta za kilimo na mifugo. Aliweka msukumo katika uzalishaji, soko na katika vyama vya ushirika. Alisimamia muswaada wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ambacho kilianzishwa kwa lengo la kutatua changamoto za kilimo nchini. Alikuwa mtanzania halisi na mzalendo. Uongozi wake uliweka msisitizo mkubwa katika kupambana na rushwa ili kuleta maendeleo kiuchumi na kijamii.

### 1.3 Kauli Mbiu na Lengo Kuu

Kauli mbiu ya kumbukizi ilikuwa ni "*Kumbukizi ya Miaka 40 ya Edward Moringe Sokoine: Urithi wa Taifa katika Uongozi Wake, Bidii, Uadilifu na Uaminifu*."Lengo kuu la kumbukizi na mdahalo huu ilikuwa ni kuenzi mchango wa Hayati Edward Moringe Sokoine katika uongozi, maendeleo ya kilimo, na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Mdahalo huu ulilenga kuwafahamisha wananchi na kizazi kipya kuhusu uzalendo, uadilifu, na uchapa kazi wa Sokoine.

### 1.4 Jinsi Mdahalo Ulivyoandaliwa

Mdahalo uliandaliwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na ulifanyika katika kampasi ya Edward Moringe, manispaa ya Morogoro. Washiriki walijumuisha wachokoza mada mashuhuri, viongozi wa serikali, watafiti, wanataaluma na watumishi wengine wa sekta ya umma, wanafunzi, wananchi, wawakilishi wa vyuo vikuu, taasisi mbalimbali, asasi za kiraia, na vyombo vya habari. Wachokoza mada walikuwa: Mhe. Anna S. Makinda, Prof. Issa G. Shivji, Mhe. Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba, na Prof. Kalunde P. Sibuga. Mada zilizojadiliwa zimeoneshwa katika jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Mada zilizojadiliwa**

| Na | Mada | Wachokoza Mada |
|---|---|---|
| 1. | Sokoine na Uongozi | Mhe. Anna S. Makinda |
| 2. | Sokoine: Uongozi na Maendeleo | Prof. Issa G. Shivji |
| 4 | Sokoine: Kilimo na Maendeleo | Prof. Kalunde P. Sibuga |
| 3. | Sokoine na Maendeleo ya Kilimo Nchini | Mhe. Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba |

Mdahalo ulifanyika kwa njia shirikishi, ambapo washiriki walipata fursa ya kujadili na kubadilishana mawazo kuhusu urithi wa Hayati Sokoine na mchango wake kwa taifa.

## 2.0 Mada Zilizojadiliwa

### 2.1 Sokoine na Uongozi

Mada hii iliwasilishwa na Mhe. Anna S. Makinda, Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2010-2015), ambaye alikuwa mmoja wa mawaziri wa mwisho aliyefanya kazi na Sokoine. Katika wasilisho lake, Mhe. Makinda alitoa uchambuzi wa mchango wa Sokoine katika uongozi na maendeleo ya Tanzania. Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu yaliyotolewa katika wasilisho lake:



***Mhe. Anna S. Makinda***

Hayati Edward Moringe Sokoine alikuwa Waziri Mkuu katika kipindi kigumu sana kiuchumi na kijamii. Nchi ilikuwa na uhaba mkubwa wa chakula na bidhaa nyingine nchini. Hata uchakataji wa chakula ulikuwa mgumu kutokana na uhaba wa mafuta. *"Kulikua hakuna kitu; kule Temeke watu walikua wanapanga mawe kwenye foleni ya chakula. Kulikua na RTC ambao ndio walikua wanaleta chakula lakini wajanja wakawa wanachukua chakula toka RTC kufanya ulanguzi."* Katika juhudi za kukabiliana na hali hiyo, ilifanyika operesheni ya kupambana na walanguzi na wahujumu uchumi, iliyojulikana kama vita ya uhujumu uchumi. Matokeo ya vita hii yanahitaji utafiti wa kina kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadae.

Baadhi ya sifa ambazo Sokoine anatajwa kuwa nazo ni nidhamu ya kazi na uadilifu, hakupenda umbea, alikuwa mkarimu, mwenye huruma, na mcha Mungu. Pia alifanya kazi bila kuchoka usiku na mchana. Sifa hizi ni sifa ambazo kila kiongozi anatakiwa kuwa nazo ili kuchochea maendeleo kiuchumi na kijamii. Mada hii iliibua mitazamo mbalimbali kwa washiriki juu ya uongozi wa Sokoine, ikionesha jinsi alivyokuwa na mvuto mkubwa kwa viongozi na wananchi kwa ujumla.

## 2.2 Sokoine na Uongozi na Maendeleo

Mada hii iliwasilishwa na Prof. Issa Shivji, Profesa Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye kwa nyakati tofauti ameandika machapisho kadhaa kuhusu Sokoine. Akiwa mchokoza mada wa pili, Prof. Shivji alifanya tafakuri kuhusu namna falsafa ya uongozi ya Sokoine ilivyochochea maendeleo nchini. Yafuatayo ni mambo makuu yaliyobebwa katika wasilisho hilo:



***Prof. Issa G. Shivji***

### (i) Kujitosheleza kwa Chakula kama Taifa

Sokoine alisisitiza kuwa nchi haiwezi kuwa huru endapo haijitegemei kwa chakula. Huwezi kujiamulia mambo yako mwenyewe ikiwa unategemea chakula kutoka nje. Kujitosheleza kwa chakula kunalinda uhuru wa taifa. Ili kufikia hali hii, lazima ulimaji na uzalishaji wa mazao ya chakula upewe kipaumbele. Sera zote zinazohusu mazao ya kilimo zinapaswa kulenga kushawishi uzalishaji wa chakula. Masuala kama ujenzi wa maghala, upangaji bei, na usafirishaji wa chakula yanapaswa kuelekezwa kwenye kuwezesha taifa kujitosheleza kwa chakula. Hata hivyo, itikadi ya Uchumi Huria imeathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa mashambani na viwandani, na hata kuathiri uchumi wa nchi na maisha ya watanzania.

### (ii) Kujitegemea kama Nchi

Sokoine aliona umuhimu wa kuhakikisha maeneo mbalimbali ya nchi yanategemeana badala ya kila kaya, kijiji, au mkoa kujitegemea. Alisisitiza kuondolewa kwa vizuizi barabarani vinavyozuia chakula kusafirishwa kwa uhuru kwenda maeneo mbalimbali.

### (iii) Kujenga na Kukuza Soko la Ndani

Sokoine alijikita katika kujenga soko la ndani au soko la kitaifa. Alisisitiza kuwa soko la ndani liwe huru, huku soko la nje likidhibitiwa. Soko huria la ndani lingechangamsha uchumi na kuwa kiungo kati ya sekta na sekta, kujenga mtandao wa kubadilishana bidhaa na kuchochea uzalishaji. Kudhibiti soko la nje kungezuia soko la ndani kuwa dampo la bidhaa za nje, jambo ambalo lingeathiri bidhaa za ndani kutokana na kushindwa kuhimili ushindani. Maono ya Sokoine yalilenga kusaidia taifa kuondokana na hali ya kuzalisha tusichotumia na kutumia tusichozalisha.

Kwa ujumla, mtazamo wa Sokoine ulikuwa kujenga uchumi wa kitaifa ulio huru kwa kuwajibika kwa mantiki ya ndani na kuondokana na uchumi wa kikoloni ambao taifa lilikua limerithi. Ingawa Sokoine alikuwa na imani na mchango wa sekta binafsi katika maendeleo, kama alivyoanzisha daladala katika jiji la Dar Es Salaam, hakuamini kwamba uwekezaji wa nje ungeleta maendeleo ya kimapinduzi aliyodhamiria.

Washiriki walikuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu jitihada za Sokoine, zikiwemo kurasimisha daladala Dar es Salaam na kuhusu kufunguliwa kwa mpaka wa Tanzania na Kenya.

### 2.3. Sokoine: Kilimo na Maendeleo

Mada hii iliwasilishwa na Prof. Kalunde P. Sibuga, Profesa wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Kama mchokoza mada wa tatu, Prof. Sibuga alifanya uchambuzi wa kina kuhusu mchango wa Sokoine katika maendeleo ya kilimo. Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyobebwa katika wasilisho hilo:



***Prof. Kalunde P. Sibuga***

#### (i) Uzalishaji katika Kilimo

Sokoine aliamini kwamba nchi ingeendelea kupitia kilimo cha mazao, mifugo (ya nchi kavu na majini), na misitu, akisisitiza kuwa kijiji ndio kitovu cha maendeleo. Alikataa wazo la mkulima kujiona maskini, na badala yake alihimiza kila mkoa kushiriki kikamilifu katika uzalishaji na kuhamasisha uchapa kazi.

#### (ii) Usafiri na Usafirishaji

Sokoine hakuweka msukumo katika uzalishaji pekee, bali pia alisimamia maendeleo ya usafiri na usafirishaji. Kwa mfano, aliamuru farasi waletwe nchini kusaidia usafiri. Mwaka 1983, alitangaza bungeni azimio la serikali kupunguza kodi kwenye magari makubwa na pick-up, azimio ambalo lilikuwa chimbuko la maendeleo ya usafiri na usafirishaji nchini, ambapo wananchi wengi walinunua pick-ups ili kusaidia usafirishaji wa mazao.

#### (iii) Ushirika na Masoko

Sokoine aliona ushirika kama nyenzo muhimu katika maendeleo ya kilimo. Alipoingia madarakani kama Waziri Mkuu, ushirika ulikuwa unatetereka, hivyo aliwahimiza wanachama kuunda vyama vya ushirika vya kidemokrasia, vinavyoanzia chini kwenda juu, na kujikita katika utafutaji wa masoko na uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo. Pia aliamini katika soko huria kwa mantiki inayoelezwa vizuri katika wasilisho la Prof. Shivji. Washiriki walijadili na kuchangia kwa undani mada iliyowasilishwa na Prof. Sibuga. Waliongeza maoni juu ya umuhimu wa kuendeleza kilimo kupitia ushirika imara, kuboresha miundombinu ya usafiri, na kuhamasisha uzalishaji endelevu vijijini. Pia, walisisitiza umuhimu wa kuwa na soko huria linalowezesha wakulima kupata bei nzuri ya mazao ya kilimo.

### 2.4. Sokoine na Maendeleo ya Kilimo Nchini

Mada hii iliwasilishwa na Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, ambaye alifanya kazi kwa karibu sana na Sokoine. Akiwa mchokoza mada wa nne, Warioba alifanya uchambuzi wa uongozi wa Sokoine na mchango wake katika maendeleo ya kilimo. Yafuatayo ni mambo makuu yaliyobebwa katika wasilisho hilo:



***Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba***

Sokoine alikuwa muadilifu, mwenye nidhamu, na mchapa kazi. Alipinga vikali rushwa na ufisadi. *"Tulikuwa tunafanya kazi pamoja; maono yetu yalikuwa yanafanana hasa kwenye masuala ya rushwa na ufisadi."*

Haiba ya Sokoine ilitokana na namna alivyoandaliwa. *"Aliandaliwa na jamii ya Kimasai na Chama cha TANU kuwa muadilifu na mwenye nidhamu. Jamii ya Kimasai ilikuwa inaandaa watu wake mpaka inaona mtu anafaa kuwa kiongozi ndipo wanamteua kuwa kiongozi."*

Alikubali kufanya kazi aliyoiona anaweza kuimudu bila kutafuta maslahi binafsi. Sokoine aliamini kuwa kiongozi lazima uwe na imani kuwa una uwezo wa kufanya kazi uliyopewa. Mwaka 1980 alikataa kuendelea kuongoza, alisema kwa afya yake na maarifa yake angependa apumzike kwani alijiona asingeweza kufanya kazi inavyotakiwa. Aliwahi pia kukataa nafasi ya uenyekiti wa CCM alisema yeye ni mtendaji na haielewi siasa. Pia, hakua na tamaa kabisa. *"Sijui kama tunaweza kupata kiongozi wa aina ile, ambaye hana tamaa kabisa, ni mwadilifu, na asiyefokafoka (soft spoken)."*

Mtazamo wa Sokoine kuhusu kilimo ulikuwa wa kipekee. Aliona kilimo kama njia kuu ya maendeleo. Alitaka kuhakikisha mkulima anapata mahitaji yake yote, ikiwemo zana za kilimo, mbegu, pembejeo na mbolea. Alikazania kuhakikisha nchi ina uwezo wa kujitegemea kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi.

Washiriki walisisitiza umuhimu wa maadili na nidhamu katika uongozi, wakibainisha kuwa malezi ya familia na jamii ya kimasai, na TANU yalimsaidia Sokoine kuwa kiongozi bora. Aidha, kiongozi bora lazima awe na nia ya dhati ya kuwatumikia watu na sio kujinufaisha yeye binafsi. Waliunga mkono mtazamo wake kuhusu kilimo kama nyenzo muhimu ya maendeleo na kujitegemea kwa taifa.

### 3.0. Hotuba ya Mgeni Rasmi



***Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko***

Hotuba ya Mgeni rasmi, Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko, ambaye alimwakilisha Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar, ilianza kwa shukrani kwa Mwenyezi Mungu na viongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa maandalizi mazuri. Aliainisha umuhimu wa kumkumbuka Sokoine kwa maadili yake ya uongozi, bidii, uadilifu, na uaminifu. Hotuba ililenga kuenzi mchango wa Hayati Edward Moringe Sokoine kwa kuonesha jinsi alivyokuwa kiongozi shupavu na mwenye maono makubwa kwa maendeleo ya taifa. Hotuba hiyo iligusia maeneo mbalimbali ambayo Hayati Sokoine alichangia, yakiwemo:

**(i) Uongozi na Maadili**

Mhe. Dkt. Biteko alionesha jinsi Sokoine alivyokuwa kiongozi wa mfano kwa uadilifu, bidii, na uaminifu. Alieleza kuwa Sokoine alisimama imara dhidi ya rushwa na ufisadi, akionesha mfano bora wa maadili katika uongozi. Hii inahusiana moja kwa moja na mada zilizojadiliwa kwenye mdahalo kama vile "Sokoine na Uongozi" na "Sokoine: Uongozi na Maendeleo" ambazo ziligusia umuhimu wa maadili katika uongozi bora. Alisistiza kwamba Hayati Sokoine alikuwa kiongozi asiyevumilia rushwa na alihakikisha viongozi na wananchi wanakuwa waaminifu na waadilifu, jambo ambalo limeendelea kuwa wito muhimu katika uongozi wa sasa na ujao

**(ii) Vita Dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi**

Katika hotuba yake, Mhe. Dkt. Biteko alieleza jinsi Sokoine alivyoongoza vita dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi. Sokoine alisimama kidete kukemea rushwa na kuchukua hatua kali dhidi ya wala rushwa na wahujumu uchumi. Hii ni sehemu muhimu ya urithi wa Sokoine, ambapo alihimiza uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa serikali na taasisi zake. Vita hii inaendana na kauli mbiu ya mdahalo ambayo ilisisitiza uadilifu na uaminifu katika uongozi, na umuhimu wa kudumisha misingi hiyo ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya taifa

**(iii) Kuinua Sekta ya Kilimo na Kupiga Vita Njaa**

Mhe. Dkt. Biteko alisisitiza umuhimu wa kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi wa taifa, akieleza jinsi Sokoine alivyojitahidi kuboresha sekta hii ili kuhakikisha taifa linajitosheleza kwa chakula. Sokoine alihimiza vijana na viongozi kubadilisha mitazamo yao kuelekea kilimo na kujituma zaidi katika sekta hii muhimu. Hotuba hii inawiana na mada zilizojadiliwa kama vile "Sokoine: Kilimo na Maendeleo" ambayo ilionesha juhudi za Sokoine katika kuendeleza kilimo na kuhakikisha taifa lina uhakika wa chakula. Dkt. Biteko alikumbusha washiriki kuwa kujitosheleza kwa chakula ni njia

mojawapo ya kulinda uhuru wa taifa, jambo ambalo Sokoine aliliona kuwa muhimu sana.

**(iv) Kujitosheleza kwa Chakula Kama Taifa**

Sokoine aliamini kuwa taifa haliwezi kuwa huru kama halijajitosheleza kwa chakula. Aliona kuwa ni muhimu kwa taifa kuzalisha chakula cha kutosha ili kuepuka utegemezi kutoka nje. Katika hotuba yake, Mhe. Dkt. Biteko alihimiza vijana kufanya kazi kwa bidii katika kilimo ili kuhakikisha Tanzania inakuwa na chakula cha kutosha kwa wananchi wake. Sokoine alihimiza sera za kilimo zinazolenga kuongeza uzalishaji wa chakula na kuhakikisha kuwa taifa linakuwa na ghala za kutosha kuhifadhi mazao. Hii inaendana na maono ya Sokoine na kauli mbiu ya mdahalo ambayo ilisisitiza urithi wa taifa katika uongozi wake wa bidii, uadilifu, na uaminifu

**(iv) Kupigania Maslahi ya Taifa na Maendeleo**

Dkt. Biteko alionesha jinsi Sokoine alivyotanguliza maslahi ya taifa mbele ya yake binafsi, akiwataka viongozi wa sasa kuiga mfano huo. Alieleza jinsi Sokoine alivyopigania miradi ya maendeleo kwa weledi na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora na zinazowiana na mahitaji yao. Hii inalingana na mada zilizojadiliwa kwenye mdahalo, ambapo washiriki walionyesha jinsi Sokoine alivyokuwa kiongozi wa mfano katika kupigania maendeleo ya taifa na kutatua changamoto za wananchi kwa vitendo

**(v) Jitihada za SUA na Maendeleo ya Kilimo**

Mhe. Dkt. Biteko alitoa pongezi kwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuanza kubadilisha mitazamo ya vijana kuelekea kilimo. Alisifu jitihada za chuo katika kutoa elimu na mafunzo ya kilimo ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji wa kilimo nchini. Alihimiza SUA kuendelea na juhudi hizi ili kuhakikisha maono ya Sokoine yanaendelea kutekelezwa kwa vitendo. Hii inaendana na mada za mdahalo ambazo zilionyesha mchango wa SUA katika maendeleo ya kilimo na kuenzi urithi wa Sokoine kwa vitendo

Kwa ujumla, hotuba ya Mhe. Dkt. Biteko alitoa mwanga juu ya umuhimu wa kuenzi urithi wa Hayati Edward Moringe Sokoine kwa vitendo. Ilitoa mwongozo wa namna ya kufanikisha hili kwa kuzingatia maadili ya uongozi bora, kujitosheleza kwa chakula, na kuimarisha sekta ya kilimo. Hotuba hii iliwiana kikamilifu na mada zilizojadiliwa na kauli mbiu ya mdahalo, na kutoa wito kwa vijana na viongozi wa sasa kuendeleza urithi wa Sokoine kwa vitendo.

## 4.0 Uchambuzi na Tafakuri

Kutokana na uchambuzi wa wanazuoni na wanasiasa waliofanya kazi na Hayati Sokoine au kufuatilia hotuba na utendaji wake, ni dhahiri kwamba Sokoine alikua kiongozi ambaye alifuata misingi ya uongozi na aliyejitoa kupigania maendeleo ya

kilimo na hata sekta nyingine. Haiba yake imeelezewa kama kiongozi muadilifu, mwaminifu, mzalendo, mpenda haki, jasiri na mchapa kazi. Hizi ni sifa za kiongozi bora; hata hivyo ni mara chache wanapatikana viongozi wenye sifa hizi. Hivyo, kuna sababu ya kuendelea kuchambua na kutafakari mambo yanayochangia kupatikana viongozi wenye sifa hizi na kuendelea kuhimiza uzingatiwaji wa mambo hayo.

Haiba, maono na fikra za Sokoine vimetokana na taasisi zilizohusika na makuzi yake kama vile familia yake, kabila lake, dini yake, na taasisi za elimu na siasa. Hali ya uchumi wa ndani na nje ya nchi na siasa zake pia vilichangia. Haya yanajieleza kupitia vifungu vifuatavyo, kama vilivyotoholewa kwenye mawasilisho ya wanazuoni mbalimbali katika mdahalo:

*"Sokoine aliandaliwa na jamii ya Kimasai na Chama cha TANU kuwa muadilifu na mwenye nidhamu. Jamii ya Kimasai ilikua inaandaa watu wake mpaka inaona mtu anafaa kuwa kiongozi ndipo wanamteua kuwa kiongozi".*

*"Maadili hayafundishwi chuoni au shuleni; uadilifu unatokana na unavyolelewa shuleni na nyumbani. Huwezi kufundisha uongozi ukasema atakaepata maksi za juu ndie kiongozi; hapana. Kuna values; kipimo ni jamii yenyewe. Maandalizi makubwa ya vijana ni sisi tunavyoishi. Huwezi kusisitiza uadilifu wakati wewe sio mwadilifu. Msifikiri viongozi watakaokuja watakuja na values tofauti na hivi tunavyoishi".*

Maono na fikra za Sokoine, kama yanavyojidhihirisha kwenye hotuba zake, yalijikita kwenye kujitosheleza kwa chakula kama taifa, kujitegemea kama nchi, na kukuza na kujenga soko la ndani.

Kujitosheleza kwa chakula ni jambo la msingi toka enzi za Sokoine, hasa miaka ya 80 wakati taifa likipita katika uhaba mkubwa wa chakula, na limebakia kuwa jambo linalozingatiwa na serikali hadi leo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba uhaba wa chakula unasababisha utegemezi na hivyo kuhatarisha uhuru wa nchi. Mapinduzi ya kilimo yaliyohimizwa na Sokoine yanahimizwa mpaka leo kwani ndio njia kuleta utoshelevu wa chakula.

Katika kuweka mkazo wa soko la ndani, kuondoa vizuizi kati ya mkoa na mkoa ulilenga kuwezesha mazao kusafirishwa kutoka mikoa inayozalisha kwa wingi kwenda mikoa yenye upungufu na hivyo kurahisisha biashara ya mazao ya kilimo kupitia soko la ndani. Umuhimu wa hatua hii unaendelea kuonekana mpaka leo ambapo serikali inaendelea kusisitiza uondoaji vikwazo visivyo vya lazima, vinavyozuia usafirishaji wa mazao kati ya mkoa na mkoa.

Kuweka vizuizi mipakani wakati wa sera ya ujamaa na kujitegemea unaweza kutafsiriwa kama hatua sahihi. Hata hivyo, katika kipindi ambacho Sokoine alikua kwenye awamu yake ya pili kama Waziri Mkuu, vuguvugu la nchi kutoka kwenye mfumo wa uchumi wa kijamaa kuelekea kwenye uchumi wa soko huria lilishaanza.

Hivyo, kwa kipindi hicho na hata sasa, ambapo sera ya “uliberali mamboleo” imetawala, kuzuia wakulima kuuza mazao nje ya nchi ni kuzuia maendeleo ya taifa. Kwa mfano, serikali inasisitiza kuzalisha kibiashara, sera ambayo haiendani na kuweka vizuizi kuuza mazao ya kilimo nje ya nchi. Pia kuna mazao kama kahawa, korosho, mbaazi, ufuta, na mengine ambayo soko lake la ndani ni dogo na hivyo kupelekea umuhimu wa kufungua milango kwa ajili ya kuuza nje ambako mazao hayo yanahitajika. Cha msingi pia ni kuongeza thamani ya mazao haya kwa maana ya kufungamanisha sekta ya kilimo na viwanda. Hata hivyo, suala la soko la bidhaa katika nchi za kiafrika ikiwemo Tanzania bado ni changamoto kubwa ya kimaendeleo. Ipo changamoto ya ufinyu wa soko la ndani ama kutokuwepo kabisa, na pia changamoto ya ubora wa bidhaa inayozalishwa nchini ambayo hupelekea kutoaminika katika soko la ndani na nje ya nchi.

## 5.0 Hitimisho na Mapendekezo

### *5.1 Hitimisho*

Mdahalo wa kumbukizi ya miaka 40 ya Hayati Edward Moringe Sokoine ujadili kwa kina urithi wake katika uongozi, maadili, na maendeleo ya kilimo. Mada kuu zilizojadiliwa zilionesha jinsi Sokoine alivyojenga msingi imara wa uongozi wenye maadili na uzalendo, pamoja na juhudi zake za kuimarisha sekta ya kilimo kwa manufaa ya taifa.

### 5.2 *Mapendekezo*

Kwa kuzingatia uongozi wa Sokoine na mchango wake, yafuatayo ni mapendekezo ya mwelekeo wa baadaye kama yalivyojitokeza kwenye mdahalo na kutokana na uchambuzi uliofanywa hapo juu:

**(i) Kuandaa Midahalo**

Ni muhimu kujifunza kutokana na maono na fikra za viongozi kama Sokoine na kuyaendeleza yale mazuri waliyoyafanya. Njia moja wapo ni kuwa na midahalo maalumu juu ya yale waliyoyasimamia, kama vile maadili ya viongozi na watumishi wa umma, uhakika wa chakula, masoko, na vijiji kama kitovu cha maendeleo. Vyuo vikuu vinatakiwa kuchochea na kuendeleza mijadala hii.

**(ii) Kufundisha Somo la Maadili**

Maadili ni moja ya sifa kuu za kiongozi. Ingawa maadili yanatoka katika taasisi mbalimbali za kijamii kama familia, ukoo, na kanisa; kufundisha somo la maadili katika ngazi zote za elimu itasaidia kujenga fikra chanya kuhusu uongozi na kuona cheo kama dhamana.

**(iii) Kuendeleza Juhudi za Kuleta Mageuzi katika Kilimo**

Kuna tija ndogo na ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo nchini. Suala la kuboresha shughuli za ugani ni la msingi ili kuleta mageuzi katika kilimo Ingawa ni muhimu kuwa na afisa ugani katika ngazi ya kijiji na kata, na vitendea kazi vinavyotakiwa, matumizi ya teknolojia ya habari na ubunifu ni muhimu katika kilimo kama ilivyo ruzuku ya pembejeo sambamba na ongezeko la mtaji katika kilimo ili kuweza kukabiliana na changamoto kama mabadiliko ya tabia nchi na matumizi kidogo ya teknolojia yanayo sababisha kudorora kwa tija. Pamoja na ongezeko la bajeti katika Wizara ya Kilimo, bado nchi yetu kupitia wizara zinazohusiana na kilimo inahitaji kuongeza mtaji ili kuwa na matokeo chanya.

**(vi) Kusimamia Soko la Ndani na Kukuza Kilimo**

Sera za kilimo zinapaswa kulenga kushawishi uzalishaji wa chakula, kujenga na kukuza soko la ndani. Masuala kama kuongeza thamani ya mazao, ujenzi wa maghala, upangaji bei, na usafirishaji wa mazao ni ya msingi katika maendeleo. Pamoja na kuwa reli ya mwendo kasi inaunganisha mkoa kwa mkoa, barabara za maeneo ya vijijini bado zinapitika kwa msimu. Wakati wa masika barabara za vijijini hupitika kwa shida. Ni muhimu njia za usafirishaji zikaboreshwa maeneo ya vijijini ili kuwezesha wakulima kusafirisha mazao yao hadi njia ya reli, na kisha kuwaunganisha na soko la ndani.

**(vii) Kuimarisha Vyama vya Ushirika**

Vyama vya ushirika vinapaswa kuimarishwa ili kuhakikisha ushirika unakuwa na nguvu na uwezo wa kusaidia wakulima kupata masoko bora na bei nzuri kwa mazao yao. Vyama vya ushirika pia hutoa elimu kwa wakulima na kusaidia upatikanaji wa pembejeo muhimu za kilimo.

**Kiambatisho Na 1: Wachokoza Mada**

| Jina | Cheo | Wasifu |
|---|---|---|
| Mhe. Anna Semamba Makinda | Spika wa Bunge Mstaafu | Mwanasiasa maarufu aliyeitumikia TANU na CCM kwa miaka 50. Alikuwa Mbunge, Naibu Spika, na Spika wa kwanza mwanamke wa Bunge la Tanzania. Amewahi kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu. Kimataifa, alikuwa Mwenyekiti na Rais wa UNICEF. Ameongoza bodi mbalimbali nchini. |
| Prof. Issa Gulamhussein Shivji | Profesa Mstaafu wa Sheria | Profesa wa Sheria aliyefundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa zaidi ya miaka 50. Ametoa machapisho ya vitabu zaidi ya 20 na kushiriki katika kamati nyingi kitaifa na kimataifa. Amepata tuzo nyingi za kitaifa na kimataifa. |
| Mhe. Joseph Sinde Warioba | Waziri Mkuu Mstaafu | Mwanasheria na mwanasiasa maarufu aliyewahi kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Tanzania. Amewahi kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi ndani na nje ya nchi. Aliwahi kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki na Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya kupambana na rushwa. Ni Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo. |
| Prof. Kalunde Pilly Sibuga | Profesa wa Kilimo (SUA) | Profesa na mtafiti anaefundisha masomo mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na vyuo vingine. Amewahi kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi chuoni na nje ya chuo. Ameandika machapisho ya kisayansi takribani 60 na kushiriki katika miradi mingi ya utafiti. |

**Kiambatisho Na 2: Wajumbe wa Kamati ya Maandalizi**

| | |
|---|---|
| Prof. J.S. Kabote | Mwenyekiti |
| Dkt. E.T. Malisa | Katibu |
| Dkt. G.D. Massawe | Mjumbe |
| Bw. S. Mkolwe | Mjumbe |
| QS. Gorold Mng’ong’o | Mjumbe |
| Ms. Suzana Magobeko | Mjumbe |
| Bw. Bahati Mmari | Mjumbe |
| Bw. Mwamtobe | Mjumbe |

**Kiambatisho Na 3: Picha za Tukio**














SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE
'1984'
ARDHI NI HAZINA







